**LOWELL PUBLIC SCHOOLS**
Henry J. Mroz Central Administration Offices
155 Merrimack Street
Lowell, MA 01852

*Inayofuata ni wasifa kuhusu kila mmoja wa waombea watatu wa mwisho katika kazi ya Mkuu wa Shule ya Lowell High School - Ian Charles, Michael Fiato, na Sara Pragluski Walsh. Wasifu zimepangwa katika orodha ya alfabeti:*

## IAN CHARLES

Ian N. Charles alianza kazi yake ya ualimu kama mwalimu mbadala wa muda mrefu mwaka wa 1998 akihudumia jamii ya Lowell Public School katika elimu maalum, masomo ya kibinaadamu, na masomo ya jamii. Alifanya kazi katika Rogers, Robinson and Pyne Arts huku akisomea chuo kikuu cha University of Massachusetts katika Lowell jioni. Alikuwa mkaazi wa Lowell katika wakati wake ndani ya wilaya. Watoto wake walihudhuria shule ya Pyne Arts School baada ya kurudi kutoka Florida alipoendelea na kazi yake ya ualimu katika shule ya upili ya Olympia High School kama mwalimu wa historia na uchumi. Alirudi baadaye Massachusetts alipohudumu kama mwalimu wa masomo ya jamii katika shule ya Peabody Middle School iliyo Cambridge. Huku akifanya kazi katika shule ya Peabody Middle School, Bwana. Ian Charles alihudhuria chuo kikuu cha Cambridge College jioni huku akisomea usimamizi wa elimu. Aliajiriwa kama msaidizi wa mwalimu mkuu wa muda katika shule ya Healy Middle School iliyo Somerville. Aliajiriwa kikamilifu kama msaidizi wa mwalimu mkuu katika shule ya Winter Hill Community Innovation School.

Aliajiriwa baadaye na Medford kusaidia kuongoza shule ya kati ya McGlynn Middle School. Kazi yake ya kipekee kama kiongozi wa kielimu ilionekana na jamii na usimamizi wa wilaya wa Medford Public School. Akateuliwa kama msaidizi wa mwalimu mkuu wa shule ya upili ya Medford High school aliposimamia mpito wenye mafanikio wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wa shule ya upili uliyo na zaidi ya wanafunzi 325. Kazi yake pia ikaonekana na shule ya Umma katika Dorchester ambapo alihudumia baadaye kama mkuu wa shule wa Codman Academy.

Ian Nigel Charles alihitimu katika shahada lake la kwanza la B.A. katika sera ya umma na usimamizi iliyo na zingatio zaidi la sayansi ya siasa kutoka chuo kikuu cha University of Massachusetts liyo Lowell mwaka wa ’99. Bwana. Charles pia alihitimu katika shahada lake la pili la M.Ed. katika mtaala na ualimu katika Chuo Kikuu cha University of Massachusetts iliyo Lowell mwaka wa ’02. Pia ana shahada la Certificate of Advance Graduate Study (Shahada la Masomo Yaliyotangulia

Uhitimu) (C.A.G.S.) kutoka chuo kikuu cha Cambridge College mwaka wa’11 iliyo na zingatio zaidi katika sera za usimamizi na maboresho ya shule. Ian N. Charles kwa sasa ni mwanafunzi wa phd au shahada la tatu la Chuo Kikuu cha Northeastern University katika Idara ya Masomo ya Kitaaluma au College of Professional Studies katika uongozi wa usimamizi. Ana shahada ya Massachusetts ya usimamizi wa kielimu kwa darasa za 5-12. Pia ana shahada ya Massachusetts kama msimamizi wa darasa za k-12.

## MICHAEL FIATO

Michael Fiato ni kiongozi mwenye hamu na mwenye kuona mbali aliye na uzoefu wa zaidi ya miaka 20 katika elimu ya umma. Sasa hivi, Michael huhudumu kama Targeted Assistance Manager (Msimamizi wa Usaidizi Uliyolengwa) katika Statewide System of Support (Mfumo wa Usaidizi wa Jimbo zima) ya Idara ya Elimu ya Kimsingi na ya Upili au Department of Elementary and Secondary Education. Michael hushiriki na shule na wilaya zilizo na shule zilizotambuliwa kama zinazohitaji usaidizi na mwingilio katika mfumo wa uwajibikaji wa jimbo.

Kabla ya kujinga na DESE, Michael alihudumu kama Mwalimu Mkuu wa Lawrence High School, na ana ufahamu wingi wa uboreshaji wa shule, kupangiliwa upya, na ubadilishaji katika kiwango cha shule ya upili. Katika jukumu lake kama mwalimu mkuu, Michael aliongoza kuanzisha programu ya chuo kikuu cha mapema, na mwelekeo wa kazi kwa wanafunzi. Mfumo huu una programu ya uzoefu wa kazi uliyo na utendakazi wa pamoja wa sekta ya umma na ya kibinafsi na uanzishi wa mwelekeo wa kazi ambapo wanafunzi wana fursa za kuchunguza kwa makini mada maalum za mazingira ya kazi na zinazohusiana na kazi. Huku ikiendelezwa na imani kwamba wanafunzi WOTE wanafaa kupata programu zilizo na ubora wa juu wa kielimu pia alipanua fursa kupitia kupata ufadhili bora zaidi na utegemezi katika thieta, muziki na sanaa.

Kabla ya kuhudumu kama Mwalimu Mkuu, Michael alihudumu kama mkuu wa shule katika moja ya shule sita za upili za Lawrence High kwa miaka minane. Katika muda huu, shule yake ilizidisha viwango vya kuhitimu na ikapunguza viwango vya kuacha shule, na kwa uthabiti ikaboresha matokeo ya kielimu katika mfumo wa uwajibikaji wa kote jimbo. Katika historia yake ya kazi, Michael alihudumu katika jukumu tofauti kama mkuu wa kitivo, kocha wa riadha, msimamizi wa kielimu, mkuu wa shule na mwalimu mkuu. Michael hutumia hamu aliyo nayo kwa elimu ya umma, usawa na haki ya kijamii kutoka mizizi yake ya uratibu wa jamii na maendeleo ya vijana katika miaka yake ya awali ya kazi. Ana imani thabiti kwamba shule za upili zinafaa kuhakikisha wanafunzi wahitimu wakiwa na hatua ijayo kama mpango wa baada ya shule ya upili itakayowawezesha kufanikiwa katika karne ya 21.

## SARA PRAGLUSKI WALSH

Sara Pragluski Walsh, Ed.D kwa sasa huhudumu kama Mkuu wa Shule ya Upili ya Algonquin Regional High School (ARHS). Ana leseni ya kufundisha katika biyolojia na hesabu, iliyo na zingatio zaidi ya fisiolojia. Pia amehudumu katika jukumu la Mwalimu mkuu Mshiriki, Msaidizi wa Mwalimu Mkuu, na Mwalimu Mkuu katika shule za Springfield Public Schools.

Dr. Walsh ametimiza ukuaji wake wa kitaaluma kupitia kazi yake kama mpangaji wenye ustadi kwa mijengo huku akitoa fursa zaidi na uwezo wa wanafunzi wote kujiunga na masomo ya juu. Pia amefanya kazi na programu ya Turn Around and Sustainability Practices (Mazoea ya Kubadili na Endelevu) Kupitia Idara ya Elimu ya Kimsingi na ya Upili (DESE) akishinda tuzo kadhaa katika muda huu kwa maboresho yenye maana katika viwango muhimu maalum na uboreshaji wa kote shule wa jumla.

Amedhihirisha upendo wake wa masomo kwa kuhitimu shahada yake ya tatu ya chuo kikuu au PhD katika Uongozi wa Elimu na Usimamizi kutoka Chuo Kikuu cha American International College na pia ana shahada ya kiwango cha pili cha Masters of Science katika Fisiolojia ya Mazoezi kutoka Chuo Kikuu cha University of Massachusetts Amherst.

Kama Kiongozi, Dr. Walsh huelezewa kama mwenye shauku, anayepanga na kudhihirisha matarajio ya juu huku akitegemeza wengine kufanikiwa zaidi ya matarajio yao. Ana aamini na ana hamu katika elimu na mifumo akiwa mwanafunzi wa maisha. Dr. Walsh ana nia kuchangia uzoefu wa hali ya juu wa kielimu kwa washika dau wote na wenzake husifu uwezo wake wa kushiriki, kushughulika, na kuhamasisha na pia kuwasiliana vizuri.

Sanaa na shughuli zisizo kwa mtaala pia ni muhimu katika kukuza mazoefu mazuri ya kielimu ambazo hudhihirisha kupitia hamu zake za kibinafsi. Dr. Walsh ana mapenzi ya maisha kwa sanaa ambazo huziongelea kupitia mazoefu yake mazuri kama mwanafunzi katika madarasa ya sanaa, bendi, na bendi za kutembea. Hufanya kazi kuhamasisha watoto wake na mapenzi haya.

Huonyesha chanzo cha mafanikio yake mengi kutokana na uzoefu wake mzuri kama mwanafunzi wa Springfield Public Schools kutoka utofauti, utegemezi na fursa. Uzoefu huu ulimwelekeza kufunza na pia kuongoza mji wake katika muda wa awali wake wa kazi ya ualimu. Mvuto wake katika fisiolojia na hesabu umemsaidia kuboresha mazoezi yake ya riadha ambapo amestaafu kama mwanariadha wa mara tatu wa Kiwango cha Dunia wa Ironman triathlete, mshindani wa mara kumi, pamoja na mshindi wa tuzo wa mbio za marathon na ultramarathon.

Mwishowe, Dr. Walsh anatarajia fursa zinazotolewa kila siku kuwa katika sehemu ya elimu na kuongoza masomo katika mtindo uliyo na usalama, ushiriki na umoja.